**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

Shule ya Sekondari Tanga Ufundi
S.L.P 5002
**TANGA**
**19/11/2025**

SIMU NA: 0789 589 472 /0654 488483 - MKUU WA SHULE
0735 688916 /0784 688916 - MAKAMU M/SHULE
0659 417697 /0623 634039 - MATRON
0714 636 489 - PATRON

Tovuti: www.tangaschool.sc.tz
Barua pepe: tangaschool@yahoo.com

**Kumb. Na. TTS.JI./FI/2026**

Kwa: ……………………………………………….
……………………………………………….

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)**
**<u>KIDATO CHA KWANZA 2026 – SHULE YA SEKONDARI TANGA UFUNDI</u>**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na Shule ya Sekondari Tanga Ufundi, kidato cha **KWANZA 2026. KARIBU SANA TANGA SCHOOL** (Shule ya Sekondari ya kwanza ya Serikali). Ni shule ya bweni kwa kidato cha kwanza hadi cha sita. Pia ni shule ya mchepuo wa **Ufundi/Amali Uhandisi** na mchanganyiko wa wasichana na wavulana kwa kidato cha Kwanza hadi cha Nne. Aidha, ni shule yenye Tahasusi za Sayansi
(**“Subject Combinations”) PCB, PCM & PMCs** kwa Kidato cha Tano na Sita.

**Shule itafunguliwa tarehe 13/01/2026** Shule iko katika **Jiji la Tanga, eneo la Makorora** karibu na **Makorora Community Centre, Kilometa 10 kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Kange**. Kuna usafiri wa Town Bus: Kwanza kutoka Kange Bus Stand hadi (Stend ya zamani) nauli **Tshs 500/=** na pili kutoka Raskazoni kupitia Stendi ya zamani hadi Makorora Sahare-Tanga School kwa nauli ya **Tshs 500/= .** Boda boda ni kati ya **sh 2,000/=** hadi **5,000/=**

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**A. SARE YA SHULE:**

Mzazi anatakiwa kumnunulia mwanae sare ya shule kama ifuatavyo:

**(i) WASICHANA;**

1. Sketi mbili za **rangi ya Dark Blue (Na.1)**. Sketi ziwe za rinda boksi ndefu zinazofika kwenye vifundo vya miguu.
2. Shati mbili nyeupe (kitambaa kizito cha **haluwa)** za mikono mifupi na vikoti viwili vya **rangi ya Dark Blue (Na.1)** visivyobana.

**Kwa wasichana wa Kiislamu wanapaswa kuwa na: -**

3. Sketi 2 za **rangi ya Dark Blue (Na.1)**, ndefu zinazofika katika vifundo vya miguu, zenye marinda tajwa hapo juu.

4. Shoti kanzu mbili mbili 2 nyeupe (haluwa) za mikono mirefu zisizofunika viganja vya mikono, ziwe pana zisibane, pia ziwe ndefu zinazoishia juu ya magoti, isiwe kama gauni na isiwe nyepesi.

5. Hijabu jozi 2 nyeupe (haluwa) ziwe pana, ndefu na zinazositiri vizuri. Hijabu **haupaswi** kufunika viganja vya mikono, isifunike uso pia isiwe nyepesi na wala isiwe na urembo wowote.

**(ii) WAVULANA;**

1. Suruali **2** za **rangi ya Nyeusi (Na.1)**. **zisiwe za kubana** (***modo***) Suruali chini ziwe na upana wa inchi **16 au 17,** mbele iwe na rinda mbili **("Celebration**") kila upande na mifuko miwili ya **"cross",** na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kuwekea mkanda.

2. Shati mbili nyeupe (kitambaa kizito cha **haluwa)** za mikono mifupi.
3. Mkanda mweusi usiwe mpana sana wala usiwe na bakoli/chata kubwa ya kubandika.

**Mahitaji ya Pamoja**

1. Madaftari 10 makubwa (Counter books) Quire 3 au Zaidi.
2. Begi la kubebea madaftari (SCHOOL BAG) Liwe na mikanda ya kuvaa mgongoni. Lisiwe la plastiki/nailoni wala lenye maandishi makubwa au picha.
3. Kompasi (Mathematical set).
4. Kalamu, Penseli, rula, vifutio vya kutosha.
5. KAMUSI (English/Swahili) **kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kamusi yake.**
6. Rim 2 za karatasi nyeupe **A4** kwa ajili ya kuchapishia mitihani na Rim 1 ya karatasi zenye mistari (***rulled papers***) kwa ajili ya kujibia mitihani, Rim 1 ya A3 kwa ajili ya michoro na karatasi za grafu (graph papers) 1
7. Fagio la chelewa lenye mpini mrefu (wote)
8. Sabuni ya maji lita 5 (Zingatia ubora. Mf. Dexi n.k)
9. Squizer (Mopper)
10. Jembe 1 lenye mpini
11. Fagio 1 la kufuta buibui *(wasichana***)**
12. **'**Soft broom' (Wavulana**)**
13. **'**Hard broom' (Wote**)**
14. '**Ovaroli'** moja la rangi ya Dark Blue (Na. 1). Liwe na mifuko mikubwa na Ovakoti jeupe mikono mifupi.
15. Soksi nyeupe jozi 4 au zaidi (Wasichana), Walulana Soksi nyeusi jozi 4 au zaidi.

16. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visivyokuwa na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Lazima viwe vya kufunga kwa kamba.
17. Sweta 1 au zaidi la mikono mirefu ya rangi ya dark blue lenye shingo ya V.
18. Track suti ya rangi ya **light blue.**
19. Tsheti yenye **rangi ya kijivu** jozi mbili (yenye kola maarufu 'form six') itakayopigwa nembo ya shule ambayo utaruhusiwa kuivaa ndani na nje ya shule (Inapatikana duka la shule kwa gharama ya Tsh. **12,500/=)**
20. Malapa kwa ajili ya kuogea (Sio yeboyebo)
21. Sandles za rangi nyeusi kwa ajili ya kushindia nje ya Darasa.
22. Ndoo Mbili (**02**) ndogo lita 10, moja anatumia, moja akabidhi ofisini.
23. Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda (yenye alarm)
24. Kikokotoo (Calculator) casio yenye f(x) 991,
25. PPE(Personal Protective Equipments) ambazo ni Safety boots, Reflector ya rangi ya njano, Kofia ngumu, Gloves ngumu, Dust mask na Miwani ngumu kwa sababu wote watasoma masomo ya AMALI
26. Drawing board kwa ajili ya michoro mbalimbali.
27. Sanduku la Bati kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi

**N.B: Baadhi ya vifaa kama vile, madaftari, kompasi, vifaa vya usafi, Rim, ndoo na godoro vinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na shule.**

**B. MAVAZI YA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) NA MICHEZO**;

**(i) WASICHANA;**

1. Gauni mbili za kushindia (**kitambaa kizito Haluwa**) moja rangi ya zambarau na nyingine rangi ya pinki. Gauni liwe la mshono wa mwamvuli na siyo sketi na blauzi. Kwa waislamu washone hijabu zinazofanana na magauni.
2. Khanga doti moja na kitenge doti moja.
3. Viatu vya kushindia ni kobazi rangi nyeusi.

(ii) **WAVULANA;**

1. Suruali **2** za **rangi ya Khaki (Na.1)**. **zisiwe za kubana** (***modo***) Suruali chini ziwe na upana wa inchi **16 au 17,** mbele iwe na rinda mbili **("Celebration**") kila upande na mifuko miwili ya **"cross",** na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kuwekea mkanda.
2. Tsheti yenye **rangi ya kijivu** jozi mbili (yenye kola maarufu 'form six') yenye nembo ya shule ambayo utaruhusiwa kuivaa ndani na nje ya shule (Inapatikana duka la shule kwa gharama ya Tsh. **12,500/=)**.

**NGUO ZA MICHEZO KWA WAVULANA NA WASICHANA:**

Raba za michezo, jezi na bukta jozi (1) na zisiwe na maandishi au chata yoyote. Epuka kuleta jezi za timu yoyote.

**NB; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za aina nyingine tofauti na zilizotajwa hapo juu, pia perfume za aina yoyote haziruhusiwi. Akikutwa nazo atawajibishwa.**

**C. <u>MAHITAJI MENGINE:</u>**

1. Gododro la Sponji Lenye Ukubwa Wa Futi 2½X6.
2. Shuka 2 za rangi ya pink.
3. Mto na foronya 2 za rangi inayofanana na shuka
4. Chandarua kwa ajili ya kuzuia mbu.
5. Bakuli, sahani, kikombe na kijiko (**Visiwe vya plastic**)
6. Ndoo mbili za maji kwa ajili ya kuogea na matumizi mengine.
8. Sanduku moja imara la bati la kuhifadhia vitu vyako (Tranka lenye kufuli mbili)

9. Vifaa kwa ajili ya usafi wa mwili (dawa ya meno, sabuni ya kuogea, mswaki, rangi ya viatu, brashi, taulo n.k).
10. Nguo za ndani za kutosha.
11. Taulo maalumu **(Pedi)** kwa wasichana.
12. Picha 4- passport size iliyopigwa hivi karibuni (Kwa Shati Jeupe).
13. Kitambulisho cha shule (computairized) Tsh 5000/=
14. Huduma ya kuweka alama kwenye nguo zilizoagiwa pamoja na mashuka Tsh 5000

## D. VIAMBATISHO VYA KUREJESHA SHULENI.

Mwanafunzi anatakiwa akamilishe/ajaze fomu zifuatazo ambazo baadhi zimeambatanishwa.

1. Fomu **A** ya kupimwa afya. (Medical Examination form). Iwe imejazwa na Daktari wa ngazi ya Wilaya au zaidi (sio Zahanati ) na iwe ni Hospitali ya serikali.
2. Nakala (photocopy) ya cheti cha kuzaliwa
3. Fomu **B** ya taarifa binafsi. (ijazwe na mzazi/mlezi)
4. Kujaza sehemu ya kukubali kutii Sheria za shule. **"mwanafunzi ahakikishe amezisoma kwa makini na kuzielewa akiwa na mzazi/mlezi wake.Zijadiliwe kea kina"**
5. Uje na hii 'Joining Instruction' ikiwa na kurasa zote ukiwa umekamilisha vitu vyote ikiwa ni pamoja na kujaza kwa usahihi fomu zilizoambatishwa.

**MUHIMU**.

- Kukiwa na dharura ambayo inamlazimu mzazi/mlezi aje shuleni siku tofauti, dharura hiyo itashughulikiwa na ofisi ya mkuu wa shule.
- Endapo itatokea tatizo la msiba, mwanafunzi ataruhusiwa kuhudhuria mazishi ya Baba Mzazi, Mama Mzazi, Kaka au Dada wa kuzaliwa pamoja tu.
- Mwanafunzi atapokelewa shuleni akiwa amevaa sare za shule na si vinginevyo. (haruhusiwi kuja akiwa amevaa nguo za nyumbani.
- Muda wa kupokea wanafunzi ni kuanzia saa **2:00** asubuhi hadi saa **12:00** jioni.
- Shule hii ni ya Serikali, haina Dini maalum na inazingatia katiba na sheria za nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na Imani zao kwa kufuata utaratibu uliowekwa na shule. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba nyingine za shule. Tofauti na hapo mzazi /Mlezi anashauriwa kumtafutia mwanae shule inayoendeshwa kwa misingi ya dini.Mwanafunzi haruhusiwi kubadilisha dini hapa shuleni bila ridhaa ya mzazi.
- Mwanafunzi aje na fedha ya matumizi (pocket money) ambayo itatunzwa **kwa mhasibu wa shule** na kupewa kidogo kwa kusaini kadri atakavyokuwa anahitaji. **Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na fedha Zaidi ya Tsh.5,000 Bwenini.**

Uvaaji wa Sare ni **lazima kwa wanafunzi** wote wakati wa:-

(a) Masomo darasani
(b) Wanafunzi wanapotoka nje ya shule
(c) Mhadhara wa Shule (**BARAZA**)
(d) Maandamano
(e) Mikutano
(f) Mahafali ("**Graduation**")

## 3.0 MIPAKA YA SHULE

(i) Mipaka ya shule iko wazi na utakapofika hapa utaiona/utaonyeshwa
(ii) Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali cha Mkuu wa Shule
(iii) Saa za kutoka nje ya mipaka hiyo zimeonyeshwa kwenye ratiba ya shule.

## 4.0 SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA

**Ni marufuku** kuonekana sehemu zifuatazo:-

(a) Majumba ya Starehe (**Cinema Halls, Disco Halls nk**)
(b) Majumba ya kufikia wageni (**Guest Houses**)
(c) Hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila ruhusa.
(d) Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila sare ya shule
(e) Hairuhusiwi kuingia katika vilabu vya pombe na baa au 'night clubs',betting points, n.k
(f) Hairuhusiwi kuvaa makoti makubwa, makofia (Boshori) au mitandio.
(g) Haituhusiwi kuvaa pete, bangili, hereni, mikufu au kidani.
(h) Hairuhusiwi kumpeleka mgeni yeyote bwenini au kumruhusu kulala bwenini.
(i) Hairuhusiwi kwenda na ndala/yeboyebo bwaloni.
(j) Hairushusiwai kuingia chumba maalum cha walimu (Staff room) ,Ofisi za shule (school offices), Maabara, karakana na Jikoni bila kibali.

## 5.0 SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini Sheria, kanuni, na taratibu za Shule zimewekwa kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi kuelimika na kumaliza elimu yake kwa utulivu na mafanikio makubwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayevunja sheria, kanuni na taratibu hizo kwa makusudi. Hatua hizo ni pamoja adhabu ndogondogo shuleni, kusimamishwa shule na au kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa. Hivyo ni vyema kila mwanafunzi afuate sheria, kanuni na taratibu hizo kwa kutumia hekima, akili, bidii, utii busara na uaminifu ili kuepukana na uvunjifu wa sheria, kanuni, na taratibu za shule usiokuwa wa lazima.

### A. HESHIMA, USAFI NA UTUNZAJI WA MALI YA UMMA.

**Kila mwanafunzi anatakiwa**

(i) Kuheshimu Walimu na wafanyakazi wasio walimu, Wanafunzi wenzake na wanajumuiya wote.
(ii) Kushiriki kwa bidii sana katika kazi mbalimbali za Shule.
(iii) Kuheshimu ratiba nzima ya Shule bila kukosa kusanyiko lolote,vipindi vya Dini,*Preparation* zote n.k
(iv) Kila mwanafunzi atapangiwa eneo lake la kufanyia usafi kila siku na pia atakuwa na zamu ya kudeki darasa, bwalo la chakula, vyoo, na bweni lake na atatakiwa kufanya usafi kwa wakati uliopangwa.
(v) Kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote anapotakiwa na awe tayari kwa ukaguzi wakati wowote.
(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote zilizopo shuleni. Mwanafunzi atakaye haribu au kupoteza mali ya shule kwa makusudi au uzembe atawajibika kulipia uharibifu au upotevu huo.
(vii) Mwanafunzi anapaswa kuoga kwa brashi aliyoizoea (Aje nayo) angalau mara moja kwa masaa **24**. Kwa mwenye changamoto za kiafya taarifa zake zitolewe kwa daktari ili apewe huduma stahiki
(viii) Ni marufuku kupeleka chakula bwenini kwa ajili ya usalama wako na shule kwa ujumla.
(ix) Mwanafunzi anapaswa kuzungumza lugha ya Kiingereza muda wote awapo shuleni.

**NB: Atakayekiuka maelekezo haya atakabiliwa na adhabu zilizoainishwa na Serikali ya wanafunzi na kupitishwa kwenye baraza la shule**.

**B. MWANAFUNZI HARUHUSIWI KABISA KUFANYA YAFUATAYO: -**

(a) Kuvuta sigara, bangi wala madawa ya kulevya
(b) Kufuga kucha, nywele wala ndevu
(c) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama sketi fupi au suruali ya kubana
(d) Kugombana, Kutukana au kutoa lugha za matusi kwa mtu yeyote
(e) Kunyoa nywele, mitindo ya kihuni kwa mfano kipara, panki/kiduku au kusuka
(f) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule
(g) Kubeti,kucheza PS,kamari n.k
(h) Kupaka kucha rangi au kutia nywele dawa
(i) Kupaka lipstick au kutinda nyusi na kupaka wanja.

C. **MAHUDHURIO**.

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria:
(ii) Vipindi vyote vya masomo ya darasani na vya nje ya darasa.
(iii) Miito na mikutano yote k.m. Roll Calls
(iv) Kutunza muda wa ratiba nzima ya shule.
(v) Kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
(vi) Kufanya majaribio na mitihani yote atakayopewa. Akiacha kufanya mtihani/jaribio atahesabiwa kutumia rasilmali za shule vibaya na hivyo atapaswa alipe “**ream**” moja ya karatasi kwa kila mtihani aliokosa bila sababu za msingi.

D. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi
(ii) Uasherati na ushoga.
(iii) Matumizi ya kilevi cha aina yeyote.
(iv) Uvutaji wa sigara,bangi au madawa mengine ya kulevya
(v) Ubakaji na ulawiti
(vi) Makosa ya jinai
(vii) Kupiga au kupigana
(viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(ix) Kudharau Bendera ya Taifa
(x) Kuoa au kuolewa
(xi) Kumpa mimba msichana/mwanamke
(xii) Kutohudhuria vipindi vya masomo bila sababu ya msingi.
(xiii) Kukataa adhabu
(xiv) Kunyanyasa wanafunzi wengine
(xv) Kulala nje ya shule bila ruhusa maalumu
(xvi) Kuanzisha, kuhamasisha, au kushiriki mgomo na vitendo vya uvunjifu wa amani, fujo au kufanya maandamano yasiyokuwa halali/kibali.
(xvii) **Kumiliki simu ya mkononi, radio, ipad au camera**.
(xviii) Kupata ujauzito

(xix) Kutoa au kushiriki kutoa mimba

## 6.0 MAENEO YA KUFANYA KAZI.

### 6.1.0 Mabwenini.

6.1.1 Kila mwanafunzi atapangiwa na mwalimu wa bweni eneo la kufanya kazi asubuhi na jioni baada ya saa za darasani.

6.1.2 Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayeacha kuhudumia eneo lake kikamilifu. Aidha kila asubuhi/jioni mwanafunzi anatakiwa kufanya usafi katika bweni, choo, bwalo, eneo nk. Kama atakavyopangiwa na mwalimu/viongozi wake.

6.1.3 Ni **marufuku** kuwa bwenini wakati ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani/miradi/michezo/Roll-check/Baraza nk.

### 6.2.0 Darasani.

6.2.1 Wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani Kuanzia saa 1**:30 – 4:50, 5:20 – 6:40, 7:00 – 9:00** Saa **1:30** – usiku – **4:30** usiku

6.2.2 Darasa liwe safi (**lisiwe na buibui, vumbi, karatasi** nk) Mwalimu wa Darasa atakagua vyumba vya madarasa mara kwa mara. Kiongozi wa darasa na kiranja wahakikishe kila darasa ni safi. Orodha ya zamu na usafi itapangwa na Kiranja.

6.2.3 Wakati mwanafunzi akiwa darasani anatakiwa afanye yafuatayo:-

(i) Mwanafunzi asipige kelele/asitoketoke darasani bila ruhusa ya kiongozi wa darasa.

(ii) Mwanafunzi aulize na kujibu maswali

(iii) Mwanafunzi afanye test/mazoezi/majaribio yote kwa uwezo wake wote. Kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/test kwa kila somo.

(iv) Viti/madawati yapangwe kwenye mistari iliyonyooka

(v) Mwanafunzi **analazimika** kuhudhuria vipindi vyote kwa siku.

(vi) "**Private Study**" iliyopo kwenye ratiba ya siku hiyo ni **lazima** ifanyike darasani na sio nje ya darasa au mahali pengine.

(vii) Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati/taa/switch n.k. kutoka darasa moja kwenda mahali pengine. Viongozi wa wanafunzi (**monita na viranja**) wahakikishe kwamba hakuna kifaa kilichohamishwa kutoka darasa moja kwenda mahali pengine bila kibali cha mwalimu wa darasa. Ni marufuku kuunganisha umeme katika jengo lolote la shule bila kibali cha uongozi wa shule. Aidha, matumizi ya pasi na "**heaters**" bwenini hayakubaliki/hayaruhusiwi.

## 7.0 CHAKULA

**7.1** Shule inaandaa Chakula kwa ajili ya Wanafunzi wote kila Siku.Kila Mwanafunzi **ni lazima** ale chakula hicho kinachoandaliwa na shule. Chakula kiliwe ndani ya Bwalo, na ni marufuku kupeleka

chakula Bwenini au mahali pengine popote nje ya Bwalo bila **KIBALI** maalum. **Aidha, Hakuna Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule kwa ajili ya kutafuta Chakula.**

## 8.0 UTAMADUNI NA MICHEZO

### 8.1.0 Michezo

8.1.1 Shule ina michezo kama vile mpira wa miguu, wavu, kikapu, pete, meza, riadha, kuruka juu/chini na Sarakasi. Kila mwanafunzi ni **LAZIMA** ashiriki kikamilifu katika angalau mchezo mmoja. Utaratibu umeandaliwa na Mratibu wa michezo na Mwalimu Mwandamizi Malezi & Utamaduni.

8.1.2 Mwanafunzi ambaye hawezi kushiriki katika michezo hiyo awe na barua ya daktari na apewe kibali na Mkuu wa Shule.

8.1.3 Mashindano yatafanyika kila muhula na zawadi zitatolewa kwa washindi kulingana na Bajeti ya Shule.

8.1.4 Kutakuwa na Mchakachaka kila Jumamosi saa 11:30 asubuhi.

## 9.0 HUDUMA MUHIMU

9.1.0 **MATIBABU**: Shule ina Zahanati inayoongozwa na Mganga Msaidizi. Kila mwanafunzi mwenye tatizo la afya yake aingiapo shuleni atoe taarifa kwa Mganga wa Zahanati kama vile Pumu, Pressure, Kisukari, Vidonda vya tumbo nk.

9.1.1 Mwanafunzi haruhusiwi kuweka dawa bwenini. Dawa zote zikabidhiwe Zahanati ambapo mwanafunzi atapewa dawa kwa kiasi/kiwango kinachojulikana na mtaalamu wa afya.

**9.1.2** Matibabu yanatolewa kwenye Zahanati ya shule kwa utaratibu utakaoelekezwa na Uongozi wa Shule. Aidha, **kila Mwanafunzi, anatakiwa awe na Kadi ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), ili kupanua Wigo wa Huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa.** (**Gharama za Matibabu nje ya Zahanati ya Shule, zitagharamiwa na Mzazi/Mlezi**) **Gharama za (NHIF) ni 50,400/= kwa Hospitali zote zinazotumia Bima ya Afya na (CHF) ni 6,000/= kwa mwaka kwa Zahanati na vituo vya Afya Jiji la Tanga.**

### 9.2.0 Hospitali za "Rufaa"

9.2.1 Mwanafunzi atakayepimwa katika Zahanati ya shule na kugunduliwa kwamba anahitaji huduma ya ziada atapelekwa kwenye Kituo cha Afya Makorora au Hospitali ya Mkoa (**Bombo Regional Hospital**).

9.2.2 Mwanafunzi atakayezidiwa mzazi/mlezi ataarifiwa.

## 10.0 KUABUDU

### 10.1 MSIKITI

Kuna Msikiti wa Shule kwa ajili ya Wanafunzi wa Kiislamu. Msikiti huo upo hapa shuleni, kwa ajili ya Kuswali. Ni marufuku kutumia Msikiti huo kwa ajili ya **Makazi** ya Wanafunzi au Wageni.

### 10.2 MAKANISA

Madhehebu mengine yana utaratibu wa kusali katika vyumba vya madarasa na jumapili ya mwisho wa mwezi wanakwenda makanisa yaliyo karibu na Shule.

**10.3** Vipindi vya dini – Viwili kwa wiki hutolewa hapa shuleni kwa madhehebu yote. **NI LAZIMA** kila mwanafunzi ahudhurie vipindi hivyo viwili vya dini.

**11.0 HAKUNA SIKU YA KUTEMBELEA WANAFUNZI ISIPOKUWA SIKU YA MAHAFALI AU UTAKAPO TAARIFIWA NA SHULE. AIDHA TARERHE 07/03/2025 NI KIKAO CHA WAZAZI/WALEZI** UNAKARIBISHWA. Mgeni yeyote hataruhusiwa kwenda maeneo ya mabweni wala kumletea **vyakula** mwanafunzi.

12:0 **MKONDO WA AMALI/UFUNDI.**

Shule ni ya mkondo wa Amali Uhandisi kwenye fani zifuatazo.

12.1 Carpentry, Joinery and Metal works.
12.2 Mansory and Bricklaying.
12.3 Electrical Installation.
12.4 Solar power installation.
12.5 Motor vehicle mechanics.
12.6 Welding and metal fabrication.
12.7 Computer programming.
12.8 Fitter mechanics.

Hivyo mwanao anatakiwa kuchagua fani moja kati ya hizo.

14:0 **MITIHANI**

Kila muhula wanafunzi wanafanya mitihani na matokeo kutumwa kwa wazazi kupitia Tovuti ya Shule **www.tangaschool.sc.tz.** Mtoto wako ajitahidi asipate wastani wa alama **CHINI YA 50%** Kama wewe Mzazi/Mlezi hupati matokeo ya mitihani ya mwanao (kila muhula), wasiliana na Shule haraka iwezekanavyo.

15.0 **KURUDI SHULENI BAADA YA LIKIZO**

Ni jukumu la mzazi kuona kwamba mwanao anarudi shuleni siku angalau moja kabla ya siku ya kufunguliwa shule. Shule ikishirikiana na Bodi ya shule wana mikakati ya kuimarisha elimu ambapo mwanafunzi atakayechelewa kurudi kutoka likizo fupi au ndefu itabidi **AJE NA MZAZI/MLEZI WAKE**. Mwanafunzi ambaye hatakuja na **MZAZI/MLEZI HATAPOKELEWA SHULENI**..

**UKOSEFU WA MAHITAJI MUHIMU YA SHULE, ISIWE SABABU YA KUCHELEWA KUJA SHULENI.**

**15.1 MUHIMU KWA MZAZI**

(i) Tabia na mwenendo wa mtoto wako akiwa likizo ni **JUKUMU LAKO** na tutafurahi sana kama utatuandikia kuhusiana na tabia ya mtoto wako alipokuwa likizo, mema/mabaya aliyofanya, ushauri uliompa mwanao pamoja na tarehe aliyotoka nyumbani kurudi shuleni. Maelezo haya yatatusaidia sana katika malezi ya mwanao.

**N.B: Endapo Mwanafunzi atachelewa kuripoti shuleni hadi** tarehe **01/02/2026 ambayo ndio siku ya mwisho ya kuripoti, nafasi yake atakuwa ameipoteza na itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.**

HEADMASTER
TANGA TECHNICAL SCHOOL
TANGA

...................
M.M. LUZILO
HEADMASTER

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nakala: | (i) | Katibu Mkuu,<br>OR – TAMISEMI,<br>S.L.P 1923,<br>DODOMA. | - | Taarifa |
| | (ii) | Katibu Mkuu<br>Wizara ya Elimu, Sanyansi na Tekinolojia<br>S.L.P 10<br>DODOMA. | | |
| | (iii) | Maafisa Elimu wa Mikoa (Tanzania Bara) | - | Taarifa |
| | (iv) | Mkaguzi Mkuu wa Shule (K)<br>Kanda ya Kaskazini Mashariki<br>MOSHI | - | Taarifa |
| | (v) | Afisa Elimu Sekondari,<br>S.L.P 178<br>TANGA | - | Taarifa |
| | (vi) | Wajumbe wa Bodi ya Shule | - | Taarifa |
| | (vii) | Faili la Shule. | | |

**FORM A**

**TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**

P.O. BOX 5002
**TANGA**
**Date: ……**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**<u>PART A</u>**

To: Medical Officer

……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

RE: MR/MISS…………………………………………………………………………………………
(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time school course. The examination should include the following categories (I – III) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of defect. Pregnancy (category (IV) will also render a girl candidate ineligible for the course.

i. (a) Eye-sight (b) Hearing
 (b) Hearing
 (c) Limbs
  (k) Speech
  (l) Venereal Disease(s)
  (m) Leprosy
  (n) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases(s)
iv. Pregnancy

…………………
M.M. LUZILO
HEADMASTER

HEADMASTER
TANGA TECHNICAL SCHOOL
TANGA

==========================================================================

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.

i. (a) Eye-Sight…………………………………………
(b)Hearing…………………….. ……..
(c) Limbs……………………………………………..
(d)Speech……………………………… (e) Venereal Diseases……………………………. (f) Leprosy……………………………..
(g) Epilepsy…………………………………………..

ii. Neuroses…………………………………………

iii. Other Serious Disease(s)……………………..

iv. Pregnancy test…………………………………

Signature……………………………………………..Station……………………………………

Designation……………………………..Date ........................................*Delete as necessary

FOMU B

## SHULE YA SEKONDARI TANGA UFUNDI

## HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi)

1. (i) Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………………….

(**NB**. Jina hili ni **LAZIMA** liwe lile la kwenye **TSM 9** na litabaki hivyo kwa kipindi chote ambacho Mwanafunzi atakachokuwa katika Shule hii).

Shule atokayo………………………………………………………………………………….…………

(ii) Tarehe ya kuzaliwa…………………………Wilaya…………….........Mkoa….….….…………

(iii) Dini……………………………………………. Dhehebu ……………………………………

(iv) Shule ulizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Tanga Ufundi

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | JINA LA SHULE YA MSINGI/SEKONDARI | KIPINDI ULICHOSOMA |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |

Saini ya Mwanafunzi………………………………………………………………………..

2. **AFYA**

(i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliowahi kuugua mfano:TB, Polio, Kifafa nk.

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Taja matatizo ya afya yako…………………………………………………………………….

3. **JINA LA MZAZI**

(i) Mama………………………………………………*Hai/amefariki lini… ...............................?

(ii) Baba…………………………………………………*Hai/amefariki lini……………….........?

**KAZI YA**

(iii) Baba……………………………….DINI…………………………DHEHEBU…………………………

(iv) Mama……………………………..DINI…………………………..DHEHEBU……………………….

(v) Anuani ya Mzazi……………………………………………………………………………………

4. (i) Jina la atakayegharamia mahitaji ya Shule……………………………………………………………

(ii) Kazi yake ni………………………………………………………………………………………

(iii) Anuani yake ni………………………………………………………………………………

(iv) Uhusiano… ............................................. (mf. Kaka, Dada, Mjomba, Baba, Mama nk)

(v) Dini yake…………………………………..Dhehebu……………………………………………

(vi) Namba ya Simu ya Wazazi/Walezi

(i) …………………………………………………….. Uhusiano …………………………………

(ii) ……………………………………………………… Uhusiano …………………………………

(iii) …..…………………………………………………. Uhusiano …………………………………

(iv) ……………………………………………………… Uhusiano …………………………………

(v) ……………………………………………………… Uhusiano …………………………………

**5. <u>Uthibitisho wa mwanafunzi</u>**

Mimi ....................................................................................... ninakiri kuzisoma na kuzielewa Taratibu/Sheria za Shule ya Sekondari Tanga Ufundi. Hivyo ninakubali kwa hiari yangu, kujiunga na Shule ya Sekondari Tanga Ufundi na kuthibitisha kuwa, nitafuata Sheria na Taratibu zote za Shule hii, ili nitimize lengo la kuja kwangu hapa kwa manufaa yangu/familia na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakuwa kinyume na Sheria/Taratibu za Shule, nitakubali kuadhibiwa. Ninaahidi **<u>kutokuchelewa</u>** kurudi Shuleni baada ya likizo fupi au ndefu.

Saini ya Mwanafunzi……………………………………………………Tarehe……………………….

**6. <u>Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi</u>**

Mimi…………………………………………………………………ninakiri kuzisoma na kuzielewa Taratibu/Sheria za Shule ya Sekondari Tanga Ufundi. Hivyo ninathibitisha kuwa, nitampatia motto wangu mahitaji yote ya Shule, kwa lengo la kumuwezesha Mwanafunzi aliyetajwa hapo juu asome katika mazingira mazuri kwa kipindi chote atakachokuwa hapo Shuleni, kwa kuzingatia Sheria na Taratibu za Shule ya Sekondari Tanga Ufundi. Aidha ninathibitisha kuwa, yaliyoandikwa hapo juu ni sahihi. Ninaahidi kwamba, mtoto wangu hatachelewa Shule kwa kukosa mahitaji yake muhimu ya Shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi……………………………………………… Tarehe……………………………

NB: **Mzazi/Mlezi anayejaza kipengele Namba 6 hapo juu, ndiye atakayetambuliwa rasmi na Shule katika mawasiliano ya aina yoyote. Mabadiliko yoyote, yawasilishwe Shuleni kimaandishi na Mzazi/Mlezi wa awali, kupitia kwa Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji/Kata anayoishi Mzazi/Mlezi.**

*Kata isiyohusika.

***AIDHA, INASISITIZWA KUWA***:

**(1)** ***FOMU HII NI LAZIMA IJAZWE KIKAMILIFU, NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI FOMU HII, IKIAMBATANA NA FOMU A (MEDICAL EXAMINATION) NA NAKALA YA CHETI CHAKE CHA KUZALIWA KWA MAKAMU MKUU WA SHULE, WAKATI WA UDAHILI.***

***(2) MWANAFUNZI ATAKAYECHELEWA KURIPOTI SHULENI WIKI MBILI(2) BAADA YA TAREHE YA KUFUNGUA SHULE, NAFASI YAKE ITAJAZWA NA MWANAFUNZI MWINGINE.***

| Na. | SARE/KIFAA | MAELEZO | Na. | | SARE/KIFAA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. |  | Muonekano wa msichana wa kiislamu. Siketi hijabu na nusu kanzu. | 7. | |  | Miwani -Isiwe ya rangi |
| 2. |  | Sketi-Iwe ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu na kikoti | | | | |
| 3. |  | Suruali-Isiwe ya kubana yenye 'turn up' | 8. | |  | Kofia-Iwe ngumu ya rangi ya njano |
| 4. |  | Ovaroli- liwe na mifuko mikubwa | 9. | |  | Mask-Iwe inafaa kufua |
| 4. |  | Reflector-Iwe ya njano | 10. | |  | Gloves -ziwe nyeusi |
| 6. |  | Safety boot-Iwe nyeusi | | | | |